



**JAMHURI YAMUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA**



Tarehe: 25.04.2022

**TANGAZO LA ZABUNI YA UTENGENEZAJI WA NGUZO ZA  
BARABARA ZA ANUANI ZA MAKAZI.**

1. Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa imepokea Fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi la anuani za makazi.
2. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa anakaribisha maombi ya mafundi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kutengeneza nguzo za barabara kwa ajili ya anuani za makazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa.
3. Waombaji wa kazi hii wanatakiwa wawe na sifa zifuatazo;
  - (a) Aweze kufanya kazi bila malipo ya awali (advance payment)
  - (b) Awe na uwezo wa kusoma/kutafsiri mchoro.
  - (c) Awe na akaunti ya Benki.
  - (d) Awe na eneo maalumu la kufanyia kazi linalotambulika.
  - (e) Awe na vitendea kazi vya kutosha (Vifaa vya uchomeleaji vyuma)
  - (f) Awasilishe kazi za aina hiyo alizowahi kufanya na kuzisimamia.
  - (g) Uzoefu wa kazi ya uchomeleaji (Welding) usiopungua miaka 3.
  - (h) Awe na uwezo wa kuandaa mpango kazi.
  - (i) Mwombaji awe na cheti cha ufundi cha uungaji/uchomeleaji vyuma au awe amepata mafunzo katika chuo cha Ufundi VETA au vyuo vingine vya ufundi vinavyotambulika na serikali.
4. Waombaji wenye nia ya kufanya kazi hii wanaweza kupata maelekezo zaidi katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya katika Kitengo cha Manunuzi.
5. Taratibu za upatikanaji wa Mafundi zitafanyika kwa njia ya ushindani kwa kuzingatia sheria ya Manunuzi ya umma ya mwaka 2011 na marekebisho yake ya mwaka 2016.
6. Nyaraka za maombi zinapatika kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa katika Kitengo cha Manunuzi. Nyaraka za maombi zinatolewa kuanzia saa 1:30 Asubuhi mpaka saa 9:30 Alasiri siku za kazi kuanzia tarehe ya tangazo hili.